# ROHO

# MTAKATIFU

# AU UPAKO

## SHUKRANI

Namshukuru Yesu kwa kuniwezesha kutoa toleo hili la kwanza la kitabu cha  ROHO MTAKATIFU AU UPAKO Kitabu hiki namtolea Yesu na Baba yake mapenzi yake yatimie kwa walioitwa na Yesu kuwa wahubiri. Awanurukishie akili zao zipate uelewa au ufahamu juu ya kusudi lake ktk maisha yao. Asante Baba wa Yesu na Yesu pia. Amen.

**MHUBIRIWA KIMATAIFA MINISTRY, FIRST EDITION 2024**

ISBN: 1986 - 08 - 08 - 01

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki hakiruhusiwi ku-nakili, kutafsiri au kuchapishwa kwa njia yoyote bila ru-husa ya Mhubiri wa Kimataifa ministry au Mhubiri wa Kimataifa Lameck Lister. Nakuu zote zimetoka ktk bib-lia (Maandiko matakatifu in Swahili Union Version)

**MHUBIRI WA KIMATAIFA MINISTRY.**

ADDRESS: S.L.P 9332, DAR ES SALAAM

TANZANIA (EFATHA)

MOBILE: +255658601034

EMAIL: listlameck5@gmail.com

WEBSITE:www.mhubiriwakimataifa.org

ROHO MTAKATIFU AU UPAKO

1.Roho mtakatifu………………………………………

2. Upako………………………………………………..

3. Ishara ………………………………………………

4. Msaidizi……………………………………………..

5. Maombi……………………………………………

6. Anasema……………………………………………

7. Mungu………………………………………………

8. Jinsi ya kumpokea……………………………………..

9.Kuokoka……………………………………………

10. Mwisho……………………………………………

# 1. ROHO MTAKATIFU

**Roho mtakatifu** ni nani? Roho mtakatifu ni roho ya Baba yake Yesu yaani Mungu .Mungu humpa  Yeye aokokaye ili amtawale kwa huyo roho. Yesu alisema ni Msaidizi anayeishi kwa waliokoka kama mtu wa kimataifa uliyeokoka.

**"Yoh 14.16  Nami nitamwomba Baba, naye atawapa Msaidizi mwingine, ili akae nanyi hata milele;"**

Roho Mtakatifu ni Msaidizi wetu tuliokoka anayeishi nasi milele ktk wokovu. Roho mtakatifu alipewa Yesu (**Math 3: 16)** siku anaokoka alipotubu, kubatizwa na Yohana mbatizaji (mjumbe) na mitume siku ya pentekoste **Matendo 2**

Roho mtakatifu kama msaidizi hutoa msaada ktk maisha ya mtu aliyeokoka kama wewe mtu wa kimataifa uliyeokoka kwa kuomba kwa Baba yake Yesu kwa jina la Yesu:

- Kukumbusha na Kukufundisha Yote

**"Yoh 14.26  Lakini huyo Msaidizi, huyo Roho Mtakatifu, ambaye Baba atampeleka kwa jina langu, atawafundisha yote, na kuwakumbusha yote niliyowaambia."**

Roho mtakatifu hukumbusha  na kufundisha yote ya Yesu.Ukisoma injili ya Yesu (Biblia) mwombe akufundishe  naye atafanya hizo halikadhalika ukimwomba akukumbushe yale anayokufundisha au unayofundishwa na watumishi wa Yesu Kanisani.

- Kumshuhudia Yesu

**"Yoh 15.26  Lakini ajapo huyo Msaidizi, nitakayewapelekea kutoka kwa Baba, huyo Roho wa kweli atokaye kwa Baba, yeye atanishuhudia."**

Roho mtakatifu humshudia Yesu .Mtu wa kimataifa uliyeokoka ukimwomba Roho mtakatifu amshuhudie Yesu ktk maisha yako

## 2.ROHO MTAKATIFU

Ufahamu atakutumia kuzitenda kazi za Yesu au Mungu kama kuhubiri,kutenda miujiza kama kufufua mtu aliyekufa ana siku zisizozidi nne,kutoa pepo,kuponya wagonjwa(homa),kubariki watoto,kutoa Unabii na kufundisha mambo yake Yesu

- Kuwahakikishia ulimwengu juu ya dhambi,haki na hukumu.

**"Yoh 16.8 Naye akiisha kuja, huyo atauhakikisha ulimwengu kwa habari ya dhambi, na haki, na hukumu."**

Ewe mtu uliyeokoka wa kimataifa mwombe ufahamu neno hili Roho mtakatifu huuhakikishia ulimwengu juu kwa ya dhambi,haki na hukumu pale tu unapowahubiria au washuhudia habari za Yesu wengine yaani unapowaambia waokoke.Mwombe roho mtakatifu kila uendapo kumwambia (kuhubiri/kushuhudia) mtu aokoke.

Kwa habari ya dhambi kila mwanadamu ametenda dhambi kabla yakuokoka (Walio wengi),kwa habari ya haki Yesu ndiye mwenye Haki mbele za Mungu ktk historia ya maisha yake duniani tangu kuzaliwa mpaka kufa kwa kusulubiwa hakutenda dhambi na kwa habari ya hukumu ukifa ukiwa hujaokoka upo moto(kuzimu & Jehanamu) ni adhabu ya dhambi .

- Kuongoza ktk kweli.

**"Yoh 16.13 –15 Lakini yeye atakapokuja, huyo Roho wa kweli, atawaongoza awatie kwenye kweli yote; kwa maana hatanena kwa shauri lake mwenyewe, lakini yote atakayoyasikia atayanena, na mambo yajayo atawapasha habari yake. Yeye atanitukuza mimi, kwa kuwa atatwaa katika yaliyo yangu na kuwapasha habari.Na yote aliyo nayo Baba ni yangu; kwa hiyo nalisema ya kwamba atatwaa katika yaliyo yangu, na kuwapasheni habari."**

Roho mtakatifu hukuongoza mtu uliyeokoka wa kimataifa ktk kweli .kweli ni nini? Kweli ni Neno la Baba yake Yesu.

## 3. ROHO MTAKATIFU

Kweli ukuweka huru na utumwa wa dhambi kwa maana rahisi Roho mtakatifu hukuongoza usitende dhambi uyatende ya Yesu/Mungu. MwombeRoho mtakatifu akuongoze ktk kweli kila siku ili usitende dhambi utende haki ufikie utukufu wa Yesu wa kufanana wa kutoshudiwa na dhambi na watu na mungu pia ktk maisha yako duniani baada ya kuokoka mtu wa kimataifa.

- Kushauri na kupasha habari juu ya mambo yajayo.

**"Yoh 16.13 –15 Lakini yeye atakapokuja, huyo Roho wa kweli, atawaongoza awatie kwenye kweli yote; kwa maana hatanena kwa shauri lake mwenyewe, lakini yote atakayoyasikia atayanena, na mambo yajayo atawapasha habari yake. Yeye atanitukuza mimi, kwa kuwa atatwaa katika yaliyo yangu na kuwapasha habari.Na yote aliyo nayo Baba ni yangu; kwa hiyo nalisema ya kwamba atatwaa katika yaliyo yangu, na kuwapasheni habari."**

Roho mtakatifu hukushauri ushauri utokao kwa Yesu. Kabla hujaokoka pengine ulizoea ukipitia changamoto Fulani kutafuta ushauri na uliufuata ndipo ile changamoto ulishinda ee mtu wa kimataifa baada kuokoka kuna tofauti kidogo Mpe mungu nafasi hiyo kwanza ukipitia changamoto yupo roho mtakatifu ndani yako anayeweza kukushauri ushauri utokao kwa Yesu. Mwombe akushauri naye atafanya hivyo.au nenda kanisani kwa shauri kwa yale makanisa ya kuokoka yenye huduma ya ushauri.Roho mtakatifu hukupasha habari juu ya mambo ya baadaye.Mambo gani hayo? **"1kor 2:9 -10 lakini, kama ilivyoandikwa, Mambo ambayo jicho halikuyaona wala sikio halikuyasikia, (Wala hayakuingia katika moyo wa mwanadamu,) Mambo ambayo Mungu aliwaandalia wampendao.Lakini Mungu ametufunulia sisi kwa Roho"** Mfano; mtoto utayezaa,muujiza,baraka au uponyaji atakaokupa kwa kudumu ktk wokovu na kutii sauti yake.

# 4. UPAKO

Upako ni nini? Ni nguvu za mungu apewazo mtumishi wa Yesu /Mungu kwa ajili ya kazi yake aliyomtuma/aliyompeleka. Upako ni mafuta au ujazo wa Roho mtakatifu apewaye mtumishi aliyetumwa/aliyepelekwa Yesu kwa kudhihirisha kazi za mungu.

Upako Yesu huwapa watumishi wake kwa kuhudumia kanisa aliowatuma/aliowapeleka baada kukutana nao ndio wakubwa kama mitume, wainjilisti, wachungaji,waalimu,Manabii,Waandishi waliotumwa na Yesu ,waponyaji,watenda miujiza,Wahubiri wa injili.

**"Luk 4:18 Roho wa Bwana yu juu yangu, Kwa maana amenitia mafuta kuwahubiri maskini habari njema. Amenituma kuwatangazia wafungwa kufunguliwa kwao, Na vipofu kupata kuona tena, Kuwaacha huru waliosetwa,"**

Yesu alipewa Upako (ujazo wa Roho Mtakatifu pasipo ukomo) na Mungu baada ya kubatizwa na Yohana Mbatizaji kwa kazi za mungu kama zilivyoainishwa ktk maandiko hapo juu.

**"Waebr 1:9 Umependa haki, umechukia maasi; Kwa hiyo Mungu, Mungu wako, amekutia mafuta, Mafuta ya shangwe kupita wenzio."**

Maandiko haya yanasema juu ya Yesu ambaye alichukia maasi na kuipenda haki ktk maisha yake uliyoishi miaka 30 na waisraeli kabla ya kuokoka(kutubu+kubatizwa(yordani na Yohani Mbatizaji) +kujazwa Roho mtakatifu) na kupakwa mafuta ya shangwe na Mungu ndio upako kupita wenzake yaani hata Yohana Mbatizaji.

Maandiko haya yanafunua njia ya uzima ya kutafuta na kuupata upako kwa watumishi wa mungu ni kupenda haki na kuchukia maasi unatakiwa kuishi wokovu mpaka unapokubalika mbele za Yesu/Mungu.Upako hubeba karama mbalimbali za kufanikisha kusudi la Mungu na kazi zake.

## 5. ISHARA

Zipo ishara au dalili za roho mtakatifu akiwa ndani yako au ktk maisha yako zinazomtambulisha ee uliyeokoka mtu wa kimataifa.Roho mtakatifu huingia ndani mtu wa kimataifa pindi anapookoka.Zifuatazo ni baadhi yaishara za kumtambua ya yu ndani yako uliyeokoka soma ktk marko 16: 16-18.

**"Marko 16.16—18 Aaminiye na kubatizwa ataokoka; asiyeamini, atahukumiwa.Na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio; kwa jina langu watatoa pepo; watasema kwa lugha mpya; watashika nyoka; hata wakinywa kitu cha kufisha, hakitawadhuru kabisa; wataweka mikono yao juu ya wagonjwa, nao watapata afya."**

- Kutoa pepo — Mtu wa kimataifa uliyeookoka utafahamu Roho mtakatifu yu ndani yako hata kama umeokoka kwa kumhudumia nduguyo,jamaa au rafiki yako mwenye pepo na kumkemea kwa jina la Yesu . Akimtoka ufahamu Roho mtakatifu yu ndani yako na umepokea amri ya kutoa pepo kutoka kwa Yesu. Ishara hii ya roho mtakatifu hajidhihirishi pindi unapookoka ila baada ya kuokoka na kutii kile ulichoandikiwa mtu uliyeokoka.

- Kusema kwa lugha mpya — Ishara hii ya roho mtakatifu kushuka ndani ya mtu aokokaye ni ya kawaida na hutokea kwa watu wengi pindi waokokapo huongea kwa lugha za malaika.Mara nyingi hutokea papo hapo au siku chache baada ya kumpokea Roho mtakatifu.

- Wataweka mikono yao juu ya wagonjwa, nao watapata afya. — Ishara ya Roho Mtakatifu hii inahitaji kuchukua hatua pindi ulipookoka au anapookoka mtu wa kimataifa unatakiwa kutafuta

# 6.ISHARA

Mgonjwa na kumwekea mikono kwa jina la Yesu kumwombea pengine unayemfahamu kama ni ndugu,jamaa au rafiki yako ikijidhihisha kwa mgonjwa kuponywa ufahamu umeokoka mtu wa kimataifa Roho mtakatifu yu ndani yako.

Ishara hizo tukisoma ktk utatambua ni karama za Roho Mtakatifu.

**"1kor 12:8-10 Maana mtu mmoja kwa Roho apewa neno la hekima; na mwingine neno la maarifa, apendavyo Roho yeye yule;mwingine imani katika Roho yeye yule; na mwingine karama za kuponya katika Roho yule mmoja;na mwingine matendo ya miujiza; na mwingine unabii; na mwingine kupambanua roho; mwingine aina za lugha; na mwingine tafsiri za lugha"**

Ukiwa una karama mojawapo kati ya hizi ufahamu roho mtakatifu yu ndani yako na ktk maisha yako.

- Neno la Hekima
- Neno la Maarifa
- Imani
- Uponyaji
- Matendo ya Miujiza
- Unabii
- Kupambanua roho.
- Aina za lugha na tafsiri za Lugha.

7. MSAIDIZI

**“Yoh 14.16 — 17 Nami nitamwomba Baba, naye atawapa Msaidizi mwingine, ili akae nanyi hata milele; ndiye Roho wa kweli; ambaye ulimwengu hauwezi kumpokea, kwa kuwa haumwoni wala haumtambui; bali ninyi mnamtambua, maana anakaa kwenu, naye atakuwa ndani yenu.”**

Roho mtakatifu ni Msaidizi aliyetumwa kuishi ndani ya waliokoka kama wewe mtu wa kimataifa uliyeokoka. Ktk sura ya kwanza inayozungumzia roho mtakatifu nimeeleza usaidizi anaotoa roho mtakatifu ktk maisha yako mapya ndani ya Yesu (wokovu) baada ya kuokoka na jinsi ya kuomba usaidizi huo kutoka kwa Mungu.

- Kukumbusha na Kukufundisha Yote
- Kumshuhudia Yesu
- Kuwahakikishia ulimwengu juu ya dhambi,haki na hukumu.
- Kuongoza ktk kweli.
- Kushauri na kupasha habari juu ya mambo yajayo.

Ee mtu wa kimataifa uliyeokoka jifunze na kujizoeza kukesha ktk maombi ya kuomba usaidizi wa roho mtakatifu ktk maisha yako mpya ndani ya Yesu mpaka kazi zote zitakapojidhihirisha ndani yako kumbuka uliokolewa ktk dhambi uwe hodari sana kila siku isipite bila kuikabidhi kwa roho mtakatifu akuongoze ktk kweli mabadiliko uyatarajie baada ya muda kuwekwa na dhambi unazozifahamu na kuongezeka kwa amani ya kristo ndani yako.Kujzoeza kuongozwa na roho mtakatifu kwa kuomba msaada wake hukufanya kuwa mwana.

8. MAOMBI

Maombi ni nini? Maombi ni kumueleza Mungu Baba yake Yesu Mahitaji au haja za Moyo wako zinazowezekana kwako au zisizowezekana.

Mfano mke, mtoto, baraka,utajiri,furaha,amani,chakula,Mavazi

**"Yoh 15.7 Ninyi mkikaa ndani yangu, na maneno yangu yakikaa ndani yenu, ombeni mtakalo lote nanyi mtatendewa."**

Ee mtu wa kimataifa uliyeokoka ufahamu kuwa una haki ya kuomba mbele za Mungu na Kutendewa. Maombi uliyeokoka unaweza kuomba peke yako au familia yako nyumbani kwako ktk nyumba unayomiliki wewe siyo ya kupanga au na washirika wenzako waliokoka wa kanisani unakomwabudu Mungu au Yesu.

Mambo ya msingi unayopaswa kuomba mtu wa kimataifa uliyeokoka:===>

- Omba usaidizi kama nilivyoeleza ktk sura ya saba na ya kwanza

- Omba ujazwe roho mtakatifu sawa kipimo cha uwezo wa moyo wako kubeba nguvu za roho mtakatifu. Kama alivyokukusudia ktk kukuumba siku unaokoka utapewa na Mungu **Luk 11:12 –13**

- Omba chakula + mavazi + kodi kwa Yesu utapata **Luk 11:11**

- Omba hekima Yakobo 1:5

**"Lakini mtu wa kwenu akipungukiwa na hekima, na aombe dua kwa Mungu, awapaye "**

- Omba utajiri

## 9. ANASEMA

Roho mtakatifu anasema kwa njia mbalimbali anapotoa usaidizi au msaada wake kwako ee mtu wa kimataifa  uliyeokoka wakati mwingine umwombapo. Njia hizo ni:

- Kwa sauti ndani yako akisema ya Yesu.

"Matendo 13.2  Basi hawa walipokuwa wakimfanyia Bwana ibada na kufunga, Roho Mtakatifu akasema, Nitengeeni Barnaba na Sauli kwa kazi ile niliyowaitia."

- Kwa  maono ya wazi au fumbo ukiwa umelala au u macho.

Matendo 10:9 — 17  Hata Petro alipokuwa akiona shaka ndani ya nafsi yake, maana yake ni nini maono hayo aliyoyaona, wale watu waliotumwa na Kornelio, wakiisha kuiulizia nyumba ya Simoni, wakasimama mbele ya mlango,

- Maandiko matakatifu.

"1Petr 2:6  Kwa kuwa imeandikwa katika maandiko Tazama, naweka katika Sayuni jiwe kuu la pembeni, teule, lenye heshima, Na kila amwaminiye hatatahayarika."

- Kwa kutumia watumishi waliotumwa au pelekwa na Yesu

Luk 1:67— 70

Na Zakaria, baba yake, akajazwa Roho Mtakatifu, akatabiri, akisema, Atukuzwe Bwana, Mungu wa Israeli, Kwa kuwa amewajia watu wake, na kuwakomboa. Ametusimamishia pembe ya wokovu Katika mlango wa Daudi, mtumishi wake.  Kama alivyosema tangu mwanzo Kwa kinywa cha manabii  wake watakatifu;"

# 10. MUNGU

Roho mtakatifu ni Mungu sio msaidizi tu kwako bali ni Mungu pia ee mtu wa kimataifa uliiueokoka. Maandiko yafuatayo huthibitisha roho mtakatifu ni mungu mpe heshima yake sawa na Yesu na Baba yake Umhofu na kumtii utaona utendaji wa nguvu za mungu ktk wokovu wako zikikubadilisha na kukutakasa.

Roho mtakatifu ametoka kwa Mungu ambaye ni Baba yake Yesu, Roho mtakatifu ni roho yake Mungu ana asili yake. Yesu anasema ktk Yoh 14: 16-17

“”**Nami nitamwomba Baba, naye atawapa Msaidizi mwingine, ili akae nanyi hata milele;**

**ndiye Roho wa kweli; ambaye ulimwengu hauwezi kumpokea, kwa kuwa haumwoni wala haumtambui; bali ninyi mnamtambua, maana anakaa kwenu, naye atakuwa ndani yenu.”**

Roho mtakatifu ni mungu atoaye msaada kwa mtu aliyeokoka afike mahali pa kuwa huru na utumwa wa dhambi na kukuongoza kutenda haki ili akufikishe mahali pa kumpendeza mungu kwa kuyafanya mapenzi ya mungu kama Yesu alivyotenda .

Roho ni nafsi hai ya mungu kwa kuwa anaweza kusema,kuhuzunika au kufurahi.

Roho mtakatifu alishiriki ktk uumbaji wa dunia vyote vilivyomo vinavyoonekana tunasoma ktk kitabu cha

**Mwanzo 1:2**

“**Nayo nchi ilikuwa ukiwa, tena utupu, na giza lilikuwa juu ya uso wa vilindi vya maji; Roho ya Mungu ikatulia juu ya uso wa maji. “**

Ktk maandiko haya Roho mtakatifu hunenwa kama Roho ya Mungu hivyo ni Mungu kwa sababu ni muumbaji alishiriki kuumba hata wewe uliyeokoka ee mtu wa kimataifa kama tunavyosoma ktk biblia **Mwanzo 1 &2**

# 11.JINSI YA KUMPOKEA

Ipo njia ya uzima ya jinsi ya kumpokea roho mtakatifu aliye ndani yako ambayo Yesu aliipita na kufanikiwa kutenda kazi na Roho mtakatifu. Hii ndiyo njia aliyopita Yesu baada kupokea Roho mtakatifu au upako siku ile alipobatizwa na Yohana Mbatizaji au mjumbe wa mungu;

- Kufunga siku arobaini
- Kufanya kazi za Mungu  kuhubiri, kuponya n.k

Ee Mtu wa kimataifa uliyeokoka yakupasa kujifunza njia hiyo ya uzima inakupa kutunza nguvu za Mungu ulizozipokea siku ulipookoka au kubatizwa kwa maji mengi.

Unapookoka au kubatizwa kwa mengi  nguvu ya Roho mtakatifu unayoipata yakupasa uifanyie kazi kwa:

- Kufunga
- Kuomba ujue kusudi la Yesu kukuokoa
- Kwenda kufanya kazi za mungu alizofanya Yesu ukianzia na kuhuiri,kufundisha.kutoa pepo,kuponya wagonjwa na kutenda miujiza.

Kwa mtu uliyeokoka umeandikiwa ishara zitakozokutambulisha umeokoka na umemwamini Yesu Marko 16:16 ishara hizo ni

- kutoa pepo,
- kuponya wagonjwa
- Miujiza.

## 12.JINSI YA KUMPOKEA

Sio tu hatua hizo zina kufanisha kumpokea Roho mtakatifu aliye ndani yako hata upako pia kama wewe ni mtumishi wa Yesu unayejifahamu ulio ndani yako.

NB: Maishi yenye ushuhuda pia ni muhimu sana ktk kutunza hata kupokea upako au Roho mtakatifu aliye ndani yako ktk hekalu yaani mwili wako.Yesu aliishi maisha yenye ushuhuda kwa watu yasiyo na dhambi hali kadhalika mbele za mungu wa mbinguni na malaika.

Roho mtakatifu anahitaji usafi wa mwili na Roho pia utakatifu wa mwili na roho.

Usafi wa roho maana yake ni nini? Ni kupokea mambo safi yafundishwa na hekima ya mungu kwa roho mtakatifu. Mema yalimo ktk maandiko matakatifu kama baraka,miujiza au ponyaji.

Usafi wa mwili ni kuwa msafi kimwili na mazingira kama kuoga,kufua,kupiga pasi nguo , kupiga kiwi viatu au manukato, kupaka mafuta kuchana nywele, kufagia nyumba au chumba na kiwanja chake au kufyeka nyasi n.k

Utakatifu ni kutembea ktk kusudi la mungu kwa kufanya mapenzi yake au kuzitenda kazi za mungu alizozifanya Yesu ktk maisha yake duniani.

Utakatifu wa mwili ni viungo vya mwili kutumiwa na Yesu ktk kuzitenda kazi za mungu au kumtimia mungu yaani Baba yake Yesu.

Utakatifu wa Roho ni roho mtakatifu au upako ulio ndani yako kutumiwa sawa kusudi na mapenzi yake Yesu/

KUOKOKA

Kama hujaokoka ewe mtu wa kimataifa na unataka kuokoka kiri maneno yafuatayo kwa kinywa chako kwa Imani Sema,

"Bwana yesu ninakuja kwako mimi ni mwenye dhambi natubu naamini ya kwamba ulisulubiwa kwa ajili ya dhambi zangu na laana zake damu yako ilimwagika nipate ondoleo la dhambi na kupatanishwa na baba yako na ulipigwa nipate ondolewa dhambi zangu, nisamehe dhambi zangu na uniondolee bila kusahau laana zake na ulifufuka nipewe maisha mapya huru mbali na dhambi na laana zake yaani maisha ya haki na baraka Yesu ingia ktk maisha yangu na ufalme wa mungu pamoja na roho mtakatifu unipe maisha hayo ya haki yako na baraka zake pia.Andika jina langu mbinguni nijaze furaha yako ya kunisamehe na kuniondolea dhambi na laana yake na kufanyika mwana mbinguni na kupewa sehemu ya urithi wako wa kutembea na nguvu na mamlaka ya mungu wako ya kuzivunja na kuziharibu kazi za shetani ikiwepo mapepo,magonjwa n.k. Asante yesu kwa kuniokoa , kwa roho mtakatifu, kwa neema yako, kwa karama au vipawa vyako, mamlaka yako, ufalme wako na nuru yako maana umeyafanya maisha yangu kuwa na uzima wako ... Amen"

Sasa umeokoka tafuta kanisa au huduma ya waliokoka na ushirikiane nao ili upate kukua hata kufikia ufahamu wa cheo cha kristo yaliyo ktk nchi yako au bara lako lakini kama upo Tanzania karibu efatha church yapo makanisa au huduma zingine za waliokoka au Ben Hinny ministry kama upo Marekani ; Paula white ministry n.k Yesu akuongoze kwa Roho wake mtakatifu kukupeleka ktk kanisa au huduma ya waliokoka ambayo utakuwa kufikia ufahamu wa cheo cha kristo ili Yesu akutumie sawa na kusudi lake la kukuokoa.

MWISHO

Kitabu cha kuokoka kwa **mtu wa kimataifa** kipo kukupa ufahamu wa yesu uliyempokea alichokutendea yeye na Baba yake wa mbinguni mpende kwa kulitii neno lake mfano **mafundisho yake** na **nabii zake .**

Mungu alikuokoa ee mtu wa kimataifa kwa njia ya Yesu kwa kusudi uishi naye kwa njia ya Roho wake mtakatifu ufanye mapenzi yake na mwisho ufike kwake baada ya maisha yako ktk dunia.Yesu amekuandalia mahali pa kuishi nawe ndio makao matakatifu

**Yoh 14:2-3**

**" Nyumbani mwa Baba yangu mna makao mengi; kama sivyo, ningaliwaambia; maana naenda kuwaandalia mahali. Basi mimi nikienda na kuwaandalia mahali, nitakuja tena niwakaribishe kwangu; ili nilipo mimi, nanyi mwepo."**

Wewe uliyeokoka mtu wa kimataifa mwenye tumaini la kufufuliwa na Yesu ukifa leo je wajua unakiwa ufike ktk makao mahali alipokuandalia Yesu mbinguni ? Je pakoje? Tafuta na ununue Kitabu kilichoandikwa na Mwandishi aliyetumwa na Yesu kiitwacho **Kweli Mbingu Ipo?** Ukisome ufahamu Bwana Yesu alipokuandalia Baada ya Maisha Haya ukifa usipofika ufahamu hujafika.

Ukitaka kuwasiliana na Mtumishi ya Yesu Mhubiri wa kimataifa Lameck Lister :


**Tovuti:** www.mhubiriwakimaifa.org

**Baruapepe:** listlameck5@gmail.com

**Simu:** +2550658601034 or 0658601034

**Sanduku la Barua:** Efatha Church: P.o Box 35666



Mhubiri wa kimataifa Lameck Lister niliokoka mwaka 2003 kwa kuongozwa sala ya kuokoka na Paul Roberty nilipokuwa kidato cha Tatu Kibaha Sekondari nikiwa na umri wa miaka 17 ndipo nilipoupokea ufalme wa mungu.

**Mafundisho ya kukulia wokovu na Ubatizo wa maji mengi**

Mafundisho ya kukulia wokovu na ubatizo niliyapata ktk kanisa la Efatha mwaka 2003-2006. Yanahusu maisha mapya ya mtu aliyeokoka anavyotakiwa kuishi na ubatizo wa kristo. Ndani ya hayo mafundisho yanazungumzia maisha ya toba. tofauti ya maisha kabla hujaokoka na baada ya kuokoka na kile Yesu na baba yake amefanya ndani ya mtu aliyeokoka.

**Mafundisho ya Roho mtakatifu**

Mafundisho ya roho mtakatifu niliyapata mwaka 2007 ktk kanisa la Efatha - Mwenge DSM Tanzania. Na kuwekewa mkono na Mtume na Nabii Josephat . E. Mwingira mkuu na mwanzilishi wa kanisa la Efatha ili kujaa roho mtakatifu kwa upya na vipawa au karama kama ilivyo neema ya Mitume itokayo kwa Yesu kristo.

**Utumishi wa mungu**

Baada ya kumaliza mafundisho yote nimepewa cheti cha utumishi wa mungu cha ufahamu wa cheo cha kristo. Natambulikana ndani ya kanisa la Efatha kama Mtumishishi wa mungu mbele baba yake Yesu na Yesu kama mhubiri wa kimataifa. Ukitaka kuona cheti cha utumishi wa mungu nilichopata Ktk Kanisa la Efatha

Website:www.mhubiriwakimataifa.com

Email:listlameck5@gmail.com

Mobile: +255658601034 ; 0658601034